**HOTUBA.**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...**

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuruhusu tukutane hapa katika hafla hii ya uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi huu muhimu wa nyumba za watumishi wa umma hapa Dodoma, Makao Makuu ya nchi yetu.

Napenda kukushukuru kwa dhati Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Mradi huu mkubwa wa Ujenzi wa Nyumba 3,500 za Watumishi wa Umma katika eneo hili la Nzuguni, Dodoma. Naipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kuendelea kusimamia vizuri Wakala wa Majengo Tanzania katika utekelezaji wa miradi muhimu kama huu. **Hongereni sana!**

***Ndugu Viongozi, Wananchi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kuhakikisha Watumishi wa Umma wanaishi katika makazi bora, jambo ambalo litawahamasisha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Tunatambua kuwa makazi bora ni sehemu ya haki ya msingi ya wafanyakazi. Nchi nzima ina watumishi wa umma wapatao laki tano (500,000) ambao ndio walengwa wa nyumba za Wakala wa Majengo Tanzania. Hata hivyo, imeelezwa hapa kuwa hadi sasa Wakala ina jumla ya nyumba zipatazo 7,116 tu nchi nzima zikijumuishwa pia nyumba za viongozi. Hii inaonesha ni kwa kiasi gani uhitaji wa nyumba kwa watumishi wa umma bado ni mkubwa sana. Kwa hapa Dodoma, ni dhahiri kuwa baada ya Serikali kuhamishia shughuli zake zote katika Makao Makuu ya Nchi, mahitaji ya makazi pia yameongezeka. Kama ilivyoelezwa na Mtendaji Mkuu, kutokana na utafiti uliofanyika, hapa Dodoma pekee kuna uhitaji wa nyumba zaidi ya 2,000 kwa ajili ya watumishi wa Umma. Hii ndio sababu Serikali imeona ulazima wa kujenga nyumba hizi za makazi kwa watumishi wa umma hapa Dodoma na katika mikoa mingine ili kukidhi mahitaji haya. Napenda niwahakikishie watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla kuwa, Serikali itaendelea kujenga nyumba zaidi na hivyo kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inayoelekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 nchini, kwa ajili ya Viongozi wa Serikali na Watumishi wa Umma.

***Ndugu Wananchi,***

Mradi huu unategemewa kutekelezwa ndani ya miaka mitano, ambapo ujenzi ulianza mwaka jana 2021 na unategemea kukamilika mwaka 2025. Kama ilivyoelezwa na Mtendaji Mkuu, tayari Serikali imeshatoa shilingi Bilioni 14

ambayo ni sawa na asilimia mia moja ya fedha zote zilizohitajika kukamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 150 ifikapo mwisho wa mwaka huu 2022. Hali kadhalika, Serikali imeshatoa pia kiasi cha Shilingi Bilioni 1 kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba nyingine 150. Ninafurahi kuona hadi sasa mmeshafika hatua nzuri ya kukamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ambapo naamini mtaikamilisha kwa wakati kabla ya mwisho wa mwaka huu, 2022. Aidha nawapongeza kwa kuweka miundombinu ya barabara, maji safi na maji taka. Nimefurahi pia kuona mitaa yote ya eneo hili imewekwa majina na pia mmezingatia utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti na kuhakikisha mandhari inapendeza na kuvutia. Jukumu lililobaki sasa ni kuhakikisha hii miti inakua na haya mazingira yanaendelea kubaki safi. Na mimi nawahakikishia, Serikali itaendelea kutoa ruzuku na kuweka mazingira wezeshi katika ukamilishaji wa mradi huu kama ilivyopangwa.

Vilevile nawapongeza Wakala wa Majengo kwa kutekeleza mradi huu kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani; kutoa ajira kwa wakazi wa Dodoma na watanzania wengine; kufanya ubunifu na usanifu ambao umezingatia matumizi ya malighafi chache; kutumia mtambo wenu wenyewe kuzalisha zege; na kuwa na kiwanda cha kutengeneza matofali yanayotumika kwenye ujenzi wa Mradi huu. Haya yote yamechangia katika kuhakikisha mnajenga nyumba zenye ubora unaostahili kwa gharama nafuu. Aidha, nimefurahi pia kusikia kuwa mmechukua wataalam wahitimu kutoka kwenye vyuo vyetu vya ndani na kuwafunza usimamizi wa miradi na mikataba kwa vitendo. Hili ni jambo jema na la kuigwa na taasisi nyingine za Serikali.

***Ndugu Wananchi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***
Uwekezaji katika Sekta ya ujenzi ni miongoni mwa vipaumbele muhimu vya Serikali ya Awamu ya Sita. Hii ni kwa kuzingatia mchango mkubwa wa Sekta hii katika Pato la Taifa na katika kuzalisha ajira. Kwa sasa Sekta hii inakua kwa takribani asilimia 10 kwa mwaka na inachangia asilimia 15 ya Pato la Taifa. Tunafahamu changamoto bado ni nyingi katika kutekeleza Miradi kama hii hapa nchini. Kupitia hadhara hii, napenda kuwahakikishia kuwa Serikali yenu inawajali Watumishi wa Umma na itaendelea kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kama ilivyopangwa. Aidha, Serikali itaendelea kuunga mkono ubunifu na mipango ya Taasisi kama TBA kuwa na miradi mingi zaidi ya ujenzi ili kuongeza makusanyo ya ndani na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini.

***Ndugu Viongozi na Watumishi wa Wakala wa Majengo Tanzania,***
Pamoja na kazi nzuri mnayofanya, yako maeneo kadhaa ambayo hayana budi kuboreshwa. Hivyo basi, kupitia hadhara hii napenda kuelekeza mambo yafuatayo:

**Jambo la kwanza**, katika ulimwengu wa sasa hamna budi kufanya mapinduzi makubwa ya kiutendaji, kuongeza ubunifu na kujenga misingi mizuri ya kujiendesha kibiashara. Ni lazima sasa mfikirie namna ya kujijenga kibiashara ili muweze kupata mapato zaidi na kujiendesha. Hali kadhalika, hakikisheni miradi ya ujenzi inatekelezwa kwa kuzingatia ubora na ukisasa (*state of the art*), tija na kwa gharama nafuu kwa kadri iwezekanavyo.

**Jambo la pili**, ni kuhusu kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali kupitia Wizara. Serikali ilikwisharuhusu ushirikishaji wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuingia ubia. Hatua hii itapunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali pekee katika kutekeleza miradi mikubwa kama hii nchini na pia itatatua changamoto ya kuchelewa kwa utekelezaji. Hivyo, Wizara ya Ujenzi harakisheni mchakato wa marekebisho ya Kanuni za Uanzishwaji wa Wakala wa Nyumba Tanzania ili Taasisi iweze kukamilisha taratibu zote za kuingia ubia na wawekezaji.

**Jambo la tatu**, ni kuhusu wadaiwa sugu walionunua au kupangisha nyumba za Taasisi. Kumekuwa na ulegevu kwenye kufuatilia utekelezaji wa mikataba, jambo ambalo limepelekea Serikali kupoteza mapato ya kodi. Hivyo, kupitia hadhara hii nasisitiza, msimamie mikataba yenu kwa karibu zaidi. Aidha, hakikisheni pia mnasimamia na kuweka mifumo rafiki ya ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato. Fedha zisiishie mifukoni mwa watu! Kuweni wakali na mchukue hatua za kisheria haraka iwezekenavyo kwa wale wote wanaokiuka masharti ya mikataba. Msionee mtu aibu hata kama ni kiongozi!

**Jambo la nne,** napenda niwahimize Wakala wa Majengo na Taasisi nyingine kama Shirika la Nyumba la Taifa na Sekta Binafsi kujenga nyumba za makazi zitakazoendelea kuwa bora na nzuri kwa miaka mingi ijayo kwa mfano, ziwe na nafasi ya watoto kucheza, viwanja vya michezo na mazoezi, sehemu za kupumzikia pamoja na huduma muhimu za kijamii.

**Jambo la tano,** mmeeleza kuwa katika mradi huu kutakuwa na eneo la soko, maduka na vizimba vya biashara ndogo ndogo. Ninawapongeza kwa dhamira hiyo lakini nafahamu kwenye mazingira kama haya, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na upatikanaji wa maduka, nafasi katika masoko na vizimba kwa ajili ya kufanya biashara. Hivyo, ninawataka wahusika wote kuhakikisha maeneo hayo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizo za biashara yanapatikana bila upendeleo. Hakikisheni kuna uwazi katika utaratibu utakaotumika.

**Jambo la sita,** ni kuhusu matunzo ya majengo na miundombinu yote iliyopo katika mradi huu. Wekeni utaratibu shirikishi kwa lengo la kuimarisha ulinzi na

usalama wa watu na mali zao na pia kuhakikisha majengo haya yanatunzwa. Aidha, nawasisitiza Watumishi wa Umma watakaopangiwa nyumba hizi wazitunze na kuhakikisha zinabaki katika hali ya ubora wake na kutunza mazingira yanayozunguka eneo hili ikiwemo usafi na ukusanyaji taka na kutunza miti iliyokwisha kupandwa. Ninawahimiza Wakala wa Majengo Tanzania muendelee kupanda miti katika eneo ambalo bado halijaendelezwa ili punde litakapoanza kuendelezwa miti iwe imeshakuwa mikubwa. Shirikianeni na Mamlaka husika ikiwemo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ili kupata ushauri kuhusu miti bora ya kivuli, maua, matunda, dawa, viungo n.k. inayofaa katika eneo hili na mpangilio wake.

**Mwisho,** Nimefurahishwa kuona katika taarifa yenu kuwa mmepewa miradi mingine mikubwa ya kujenga majengo mbalimbali ikiwemo IKULU, Dodoma. Tekelezeni dhamana hiyo mliyopewa kwa weledi na uaminifu mkubwa ili muweze kuaminika na kupewa miradi mingi zaidi.

***Ndugu Viongozi na Watumishi wa Wakala wa Majengo Tanzania,***
Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwatakia kila la kheri katika kukamilisha mradi huu na kuwahimiza mwendelee kuchapa kazi.

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**